TANGAZO LA SERIKALI NA. 697 la tarehe 02 /12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA ITENKA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Itenka ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba WL 496 yenye majira - nukta 274370.000E, 9272374.000N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa N 08$^{o}$ 03' 38" E kwenda hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 445 yenye majira ya nukta 276236.000E, 9285550N; kwa umbali wa kilomita 13.307, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa N 35$^{o}$ 41' 08" E hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 494 yenye majira - nukta 278917.000E, 9289283.000N; kwa umbali wa kilomita 4.595, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki kwa uelekeo wa N 61$^{o}$ 28' 38" E hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 446 yenye majira - nukta 281252.000E, 9290552.00N kwa umbali wa kilomita 2.656; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S 19$^{o}$ 34' 05" E hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 702 yenye majira - nukta 282982.000E, 9285685.000N

*Tangazo la Serikali na. 697 (linaendelea)*

kwa umbali wa kilomita 5.163; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S $40^{o}$ 34’ 06” W hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 700 yenye majira - nukta 281012.000E, 9283384.000N kwa umbali wa kilomita 3.029; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki kwa uelekeo wa S $15^{o}$ 29’ 03” E hadi alama ya upimaji ya mpaka namba WL 795 yenye majira - nukta 282975.000E, 9276298.000N kwa umbali wa kilomita 7.351; baada ya hapo mpaka unaelekea katika alama ya upimaji ya mpaka namba WL 496 katika uelekeo wa S $65^{o}$ 29’ 11” W yenye majira ya nukta 274370.000E, 9272374.000N kwa kufuata Eneo la Jumla la Mbuga ya Taifa ya Katavi kwa umbali wa kilomita 9.456 ulipoanzia.”

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*